**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE MAHAFALI YA 41 YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

**UWANJA WA FURAHISHA MWANZA**
**TAREHE 24 NOVEMBA, 2022**

***Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu Mstaafu na Mkuu wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania;***

***Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda (Mb.), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia;***

***Mheshimiwa Lela Mohamed Mussa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;***

***Mhe. Meja Jenerali Suleiman Mungiya Mzee, Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mwanza;***

***Prof. Joseph Kuzilwa, Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania;***

***Prof. Elifas Bisanda, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania;***

***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya wote mliopo;***

***Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wa Vyama vya Siasa;***

***Viongozi Wote wa Serikali na Mashirika ya Umma mliopo;***

***Wajumbe wa Baraza na SENETI ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania;***

***Viongozi wa Vyuo vyote vya Elimu ya Juu mliopo hapa leo;***

***Naibu Makamu Wakuu wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania;***

***Wanajumuiya ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania;***

***Wahitimu wetu wa leo wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania na wale ambao tayari mlishahitimu;***

***Wazazi, Walezi, Ndugu, Jamaa na Marafiki wa Wahitimu wetu;***

***Ndugu wanahabari;***

***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…***

Ninayo furaha kubwa kujumuika nanyi leo kuadhimisha mahafali ya 41 ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (CKHT). Napenda kutoa shukrani kwako Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu Mstaafu na Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kunialika na kunipa heshima ya kipekee kuwa mgeni

rasmi katika Mahafali haya. Aidha, napenda kuwapongeza viongozi wote wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, wana taaluma na wafanyakazi wengine wote walioshiriki kuandaa na kufanikisha hafla hii ambayo imefana kwelikweli. **Hongereni sana!**

Nawaletea salamu za pongezi kutoka kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa wahitimu wote ambao watatunukiwa vyeti, stashahada na shahada mbalimbali kwenye Mahafali haya. Mheshimiwa Rais Samia na mimi mwenyewe tunawapongeza sana na kuwatakia kila la kheri katika fani zenu na kuwasihi mwende kuchapa kazi kwa bidii, uzalendo na uadilifu ili kuijenga nchi yetu. Tunawapongeza kwa dhati kwa kutambua kwamba ninyi ndiyo Fahari ya Tanzania.

***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, Wanachuo,***
***Wanataalum, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, katika mchakato wa kuanzisha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania alisema yafuatayo, naomba kununukuu; *". . . inawawezesha watu wazima wengi waweze kuendelea na elimu ya juu pasipo kuacha kazi zao…Kwa Nchi maskini kama Tanzania, hakuna Taasisi nyingine ya elimu ya juu inayoweza kuwa ya msaada zaidi kwa watu wetu"* mwisho wa kunukuu. Hii inaonesha ni kwa kiasi gani Hayati Baba wa Taifa alithamini sana elimu ya juu na aliiona Taasisi hii kuwa mkombozi wa wananchi wengi zaidi hususan wale walio katika ajira kupata elimu ya juu huku wakiendelea kufanya kazi zao za ujenzi wa Taifa. Nafurahi kuona kuwa, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kimeendelea kuhakikisha maono ya Hayati Mwalimu Nyerere yanatimia. Kupitia Chuo hiki tumeshuhudia jitihada kubwa za viongozi wetu kuhakikisha wananchi wanaojiendeleza wakiwa kwenye utumishi wa umma au wamejiajiri, na kundi la vijana waliomaliza kidato cha sita na ufaulu mdogo na kuamua kujiendeleza kielimu, wanapata elimu ya chuo kikuu. Mengi yamefanyika toka kuanzishwa kwa Chuo hiki, na leo tunashuhudia idadi ya wahitimu imeongezeka kutoka wahitimu wa kwanza 8, mwaka 1999 hadi kufikia wahitimu 53,698 mwaka huu 2022. Aidha, takriban 40,000 tayari wameshahitimu na wanaendelea kulitumikia Taifa katika nyanja mbalimbali. Inafurahisha kuona kuwa hata baadhi ya Viongozi Serikalini ni wahitimu wa Chuo hiki. Aidha, Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake amenikumbusha siku nilipokuwa mgeni rasmi kwenye hafla ya kufunga na kukabidhi zawadi kwa washindi wa Mashindano ya MAKISATU, ambapo Chuo hiki kilinyakuwa nafasi mbili za juu kwenye mashindano hayo. Haya yote ni uthibitisho thabiti kuwa Elimu ya Chuo

Kikuu Huria mnayotoa ni muhimu sana, na ina mchango mkubwa kwenye maendeleo ya nchi yetu. Hivyo Chuo kina kila sababu ya kujivunia mafanikio haya ambapo matunda yake yanaonekana bayana. **Hongereni sana!**

Kadhalika napenda nitumie nafasi hii pia kukipongeza Chuo hiki kwa kudahili wanafunzi kutoka katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Huu ni uthibitisho mwingine kuwa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kinatoa elimu bora inayokubalika na kutambulika kimataifa. **Pongezi nyingi sana kwenu!** Napenda kusisitiza muendelee kupanua mahusiano na nchi jirani na ushirikiano na taasisi nyingine za Elimu ya Juu za ndani na nje ya nchi pamoja na wadau husika wa sekta ya elimu kwa maslahi ya maendeleo ya nchi yetu.

***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, Wanataaluma, Wanachuo, Mabibi na Mabwana***

Duniani kote mifumo ya elimu imeendelea kubadilika kutokana na mazingira yaliyopo. Mabadiliko haya katika sekta ya elimu hayazuiliki kwa kuwa mambo mapya yanaibuka kila kukicha. Kwa sababu hiyo, Taasisi nyingi za elimu duniani zimeendelea kubadili mitaala na namna ya ufundishaji ili kuendana na mahitaji halisi. Tanzania kama nchi nyingine, hivi sasa inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika mifumo yake ya utoaji wa elimu. Elimu tuliyozoea na mifumo yake kwa kiasi kikubwa haiendani na mahitaji halisi ya sasa. Bado Vyuo vyetu vinalenga zaidi kumwandaa mhitimu kuajiriwa kuliko kujiajiri. Dhana hii inaonekana wazi kuwa haikidhi kutokana na ukweli kuwa, hivi sasa idadi ya wahitimu imekuwa kubwa ikilinganishwa na nafasi za ajira katika sekta ya umma na binafsi. Hivyo, kama Taifa hatuna budi kujitathmini upya ili tuweze kumudu mabadiliko hayo katika sekta ya elimu na kuandaa wahitimu watakaokuwa na ushindani kwenye soko la ajira katika sekta ya umma, binafsi na kimataifa na pia kuwa na uwezo wa kujiajiri. Hayati Baba wa Taifa Mwalimu J.K. Nyerere kwenye hotuba yake wakati akitunukiwa shahada ya Udaktari wa heshima ya Chuo kikuu Huria cha Tanzania mwaka 1999 alisema:

> *"Kama hatupendi kuwa wakataji kuni na watekaji maji kwa wenye elimu ya dunia hii, lazima tuingie katika mashindano hayo muhimu ya elimu kwa kuzingatia mambo matatu ambayo ni kuifanya elimu yetu iwe kwa wote, elimu yetu kuwa bora na elimu yetu kuwa yenye manufaa."*

Kwa kauli hii, Mwalimu Nyerere anatukumbusha kuwa, wakati tunafanya jitihada kuhakikisha elimu inapatikana kwa wote, ni lazima pia tuhakikishe elimu yetu ina ubora stahiki, inatuwezesha kuwa shindani na kutuletea maendeleo endelevu.

Hivyo, hatuna budi kuhakikisha elimu tunayotoa katika Vyuo vyetu, inaendana na mabadiliko ya teknolojia yanayoendelea kwa kasi na vipaumbele vyetu vya kitaifa ikiwamo ujenzi wa uchumi wa viwanda na uchumi wa buluu. Maeneo mengine yanayojitokeza sasa ni pamoja na uchumi wa kidigiti, nishati jadidifu, na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kwa mantiki hiyo, Chuo hiki pamoja na vyuo vingine vyote hapa nchini ni lazima kujipanga kutoa elimu iliyo bora na hasa inayolenga kuwajengea wahitimu uwezo wa kujiajiri na zaidi sana kuwa na ubunifu ambao utawasaidia kushiriki katika fursa zinazojitokeza na kujenga mihimili ya Taifa kiuchumi na kiteknolojia.

***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, Wanachuo,***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Ili Tanzania iweze kuwa nchi ya uchumi wa kati inayoongozwa na viwanda ni lazima kuwa na mifumo bora ya elimu hususan elimu ya juu. Hii ndio sababu, moja ya malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ni kuwepo kwa jamii iliyoelimika, na inayojifunza na kujenga uchumi imara unaoweza kukabiliana na ushindani. Halikadhalika, maendeleo ya viwanda hutegemea sana nguvukazi yenye ujuzi mahsusi ambayo itachangia katika kuongeza thamani ya bidhaa zote zinazozalishwa nchini. Hata hivyo, lazima tujitathmini kama kweli nguvukazi ya nchi yetu iko tayari kushiriki na kushindana katika soko la ajira. Kwa kuzingatia hili, Serikali imeendelea kuwekeza kwenye elimu ya juu na ufundi stadi kwa kuimarisha miundombinu, kuongeza bajeti kwenye sekta hii kila mwaka, na kuendelea kuboresha sera yetu ya elimu. Pia Serikali inaendelea kupitia upya mfumo wetu wa elimu. Napenda nitumie nafasi hii kutoa rai kwa wanazuoni wote wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na vyuo vingine vyote hapa nchini, kutumia weledi na utaalamu wenu katika zoezi hili la maboresho ya elimu. Mchakato huu unahitaji ushirikishwaji wa hali ya juu wa kila sekta ikiwemo Vyuo Vikuu. Ni matarajio yangu mtajiandaa kutoa mawazo yenu kwa uwazi pale itakapohitajika kufanya hivyo ili tuweze kupata mfumo ambao utakuwa halisia kwa mazingira ya sasa.

Aidha, kwa kuwa Chuo hiki ni cha kimkakati, Serikali inakiangalia kwa jicho la karibu sana. Ndio maana Chuo hiki kimejumuishwa katika mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ili kiweze kuwafikia wanafunzi wengi zaidi. Kwenye taarifa yake, Mwenyekiti wa Baraza amesema Chuo kimewasilisha andiko Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia linalohusuhu uanzishwaji wa Maabara za Sayansi kwenye Kanda Saba za Chuo chini ya ufadhili huu. Mheshimiwa Waziri wa Elimu, hakikisha unafuatilia andiko hilo na kulifanyia kazi mapema iwezekanavyo. Na

kwa upande wa Chuo, ninawahimiza mhakikishe mnasimamia vizuri mradi huu utakapoanza ili tuweze kujikita zaidi kwenye utafiti na uvumbuzi.

***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,***

Pamoja na changamoto zilizopo, napenda niwahakikishie kuwa, Serikali imejipanga kuona sekta ya elimu inaboreshwa zaidi ili kukidhi mahitaji na kuweza kuendana na jitihada za kuleta maendeleo endelevu nchini. Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya Vyuo vyetu na kuongeza idadi katika mikoa yetu yote ili wananchi zaidi wapate fursa ya kujiendeleza kimasomo na kupata elimu ya juu. Nafahamu kadri tunavyoendelea kuongeza idadi ya Vyuo, changamoto pia zinajitokeza. Mmeeleza hapa kati ya changamoto zinazowakabili ni pamoja na uchache wa wanataaluma wazoefu wenye Shahada za Uzamivu. Napenda niwahakikishie kuwa, changamoto hii inafanyiwa kazi na Serikali tayari imepata fedha za kuwaendeleza wanataaluma katika ngazi za uzamili na uzamivu. Hivyo, nawasihi wanazuoni wote wenye sifa kuchangamkia fursa hii pindi nafasi zitakapotangazwa.

Kwa kuzingatia kuwa utoaji wa elimu huria na masafa unategemea mifumo bora ya TEHAMA, Serikali ina mpango wa kuhakikisha Vyuo vyote vya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania vinaunganishwa kwenye mkongo wa Mawasiliano wa Taifa. Mheshimiwa Waziri umelizungumzia hili, lakini nakuagiza muongeze kasi ya kuunganisha vituo hivi ili kupunguza gharama za uendeshaji. Kutokuwa na mifumo imara ya TEHAMA katika Vyuo hivi kunakinzana na dhana nzima ya kutoa elimu huria na masafa.

***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, Wahitimu wetu, Mabibi na Mabwana***

Ninapohitimisha hotuba yangu napenda kuwaasa wahitimu watakaopokea vyeti leo hii. Serikali inatambua mchango mkubwa ambao umekuwa ukitolewa na Chuo hiki. Chuo kimeendelea kutoa wataalam ambao wengi wameingia kwenye sekta mbalimbali za uzalishaji na huduma na kutoa mchango muhimu sana kwenye maendeleo ya nchi yetu. Hata hivyo, tunaposherehekea mahafali haya ya 41 inabidi pia tuendelee kujitathmini kuhusu hatima ya elimu tuliyopata na hasa tutakavyo itumia kuongeza tija.

Napenda niwakumbushe kuwa, vyeti mtakavyotunukiwa ni tuzo halali kwa jitihada mlizoonesha katika masomo yenu. Baada ya hapa, jamii ya watanzania inategemea kutoka kwenu utendaji bora Zaidi, uzalendo, uadilifu na ufanisi katika fani zenu itakayoakisi viwango vilivyoainishwa kwenye vyeti vyenu. Vilevile, tunatarajia muoneshe ujuzi wa hali juu, uvumbuzi (*innovation*), ubunifu

(*creativity*), na ujasiriamali (*entrepreneurship*) katika kazi zetu na mazingira yanayowazunguka. Nawasisitiza sana mkadhihirishe tuzo zenu hizo katika utendaji wenu wa kazi na maisha yenu ya kila siku, iwe ni katika sekta rasmi au sekta isiyokuwa rasmi. Lazima muoneshe tofauti katika kutafuta majibu ya maswali mbalimbali yanayowakabili Watanzania katika jitihada zao za kujiletea maendeleo. Vyeti vyenu na shahada zenu zisiishie kwenye karatasi. Aidha, msichoke kujiendeleza Zaidi maana elimu haina mwisho.

**Baada ya kusema hayo naomba sasa nimalize hotuba yangu kwa kuwatakia kila la kheri wahitimu wote mtakaotunukiwa Shahada na Vyeti katika mahafali haya ya 41 ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.**

**Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania**
**Asanteni Sana kwa Kunisikiliza**